REUNION DES EVEQUES DU SHABA ET DU KASAI DU 15 AU 20 JANVIER 1973

SUR LES PROBLEMES DE LA JAMAA

## DIRECTIVES PASTORALES

(Traduction en swahili)

Wandugu na waana wapenzi katika Kristu:

Tarehe mwezi wa saba wa mwaka 1971, "COMITE PERMANENT" wa Waaskofu wa Zaïre walikusudia Waaskofu wote wenyi kundi la JAMAA katika jimbo lao, wakusanyike kwa kutafuta pamoja njia kwa kutengeneza mambo yenyi kutoka katika kundi lile. Wakipatana, wataweza koona pamoja njia kwa kutengeneza na kuchunga JAMAA. Walipashwa kupatana pa Kinshasa ta-rehe siku 8, 9, 10 ya mwezi wa kwanza wa mwaka 1972. Lakini mambo mingi iliwazuia. Katika mkusanyo wa Waaskofu wote wa Zaïre mwezi wa pili na wa tatu wa mwaka 1972, waliomba mara ingine, na walikusudia mkusanyo hayo.

Sasa tarehe mwezi wa kumi wa mwaka 1972, "COMITE PERMANENT" alifunga ya kama mkusanyo hayo utakusanyika pa Lubumbashi, tarehe siku ya mwezi 15 mpaka siku ya mwezi 20 ya mwezi wa kwanza wa mwaka 1973, kwa kutafuta njia moja kwa kuchunga kundi la JAMAA katika umoja na kundi la Eklezya.

Sisi Waaskofu, wachungaji wa kundi la wakristu, tunakusu-dia kukomesha uzima wa Mungu katika ushirika wa wakristu. Kazi zetu si kuzimia Roho Mtakatifu, bali kulijaribu kundi, lipate kuzaa matunda mema mingi (L. G. n° 12). Kwa ajili hiyo, sisi Waaskofu, kwa jina la "COMITE PERMANENT", tunawaonyesha njia moja kwa makundi yote ya wajamaa. Tunaomba fasi yote, ambao tupo na kundi la JAMAA, wapate kufuata namna moja mi-pango tunavofunga sasa.

Wandugu na waana wetu wapenzi katika Kristu:

Sisi wote tunajua kabisa mema gani kundi la JAMAA limezaa. Fasi yote wajamaa wameonyesha na nguvu roho ya sala, na mfano wa masai-diano ya kikristu. Wajamaa wametengeneza na kuwaponyesha umoja wa manyumba mingi sana. Kwa ajili ya mifano na mafundisho yao, wakristu wengi wame-tengeneza ndoa yao katika Kristu.

Kweli, katika nchi yetu Roho Mtakatifu alimwaga vipaji vyake.

Kwa nguvu hiyo, Bwana Yesu aliweza kulikomesha na kulion-gezeka kundi la wakristu katika hali ya kiafrika.

Kwa ajili ya kazi ya JAMAA, tunaona nyumbani bibi anageuka mwenzi wa kweli wa bwana wake; zoezo ya kutoleana mawazo na kuhurumiana nyumbani iliunganisha na zaidi mapendo ya ndoa; roho ya kusali Mungu ka-tika mambo yote ya maisha yao, ilionyesha ya kama imani inazidishwa. Namna wajamaa wanasaidiana na kutulizana wenyi uzuni, hasa katika kilio, ilikuwa alama ya mapendo kwa wakristu wa paroisse yote. Mafundisho na maadibisho ya JAMAA iliweza kuwasaidia wakristu kuacha bila woga kutumia madawa na madesturi isivokupatana na mafundisho ya Bwana Yesu.

Mifano ya masaidiano katika Eklezya: kuwapokelea wageni; kusikiliza na kubeba magumu ya wenzao; namna wajamaa walionyesha ya kama kuwa mkristu si michezo; namna walisaidia mapadri wapate kusikiliza na kuwapokelea wakristu: ile yote ni mifano ya mapendo ya Bwana Yesu. Na "Vatican II" anatufundisha ya kama mapendo ni amri kubwa ya utakatifu wetu kwa kuweza kubadilisha na kuponyesha dunia (L. G. n° 38).

Tunafurahi pa kuona kazi gani kundi la JAMAA liliweza ku-tumikia katika Eklezya ya Zaïre, na ya kama imani ya kikristu iliota mi-zizi ya kweli katika nchi yetu.

Kazi hizo si uzazi tu ya wababa na wamama; ni uzazi wa Bwana Yesu mwenyewe na Eklezya yake.

Halafu, wandugu na waana wapenzi katika Kristu, hatukosi kujua vilevile ya kama Waaskofu wa Eklezya ya Zaïre wako na magumu ya kweli, maneno ya fujo iliyoonekana katika JAMAA, sababu ya mbegu mbaya lenyi kuzaa mafundisho na tabia isiyo kupatana na mafundisho na tabia ya wakristu wa Eklezya ya Bwana Yesu.

Hatutaki kuua mema ya JAMAA na kuzimia kazi ya Roho Mtakatifu, bali maneno hayo tunapashwa kulijaribu kwa kulisafisha kundi lile.

Ndiyo maana tunapashwa kukumbuka:

1.- Ya kama Eklezya ya Zaïre yupo na magumu mengi sana. Zaidi na zaidi wakristu wote wanapashwa kupatana wote pamoja kwa kuzidisha imani, kuzaa utakatifu, na kuendelesha kazi ya kitume ya kundi nzima. Kwa hayo, tunaomba kwa nguvu wajamaa wasijitenge na wakristu wengine. Wanapashwa kuungana katika umoja wa kundi la Paroisse, pamoja na m padri, kwa kutumikia, kuendelesha, kukomesha ushirika wa wakristu, na kuleta nguvu mpya katika Eklezya yetu ya Zaïre.

2.- Sisi Waaskofu, tumeona katika kundi lenu matabia na mafundisho isiyo katika njia; nyinyi wenyewe pengine kati yenu hamuoni peupe bado. Kwa sababu hiyo tunawaamuru:

   a) Padri, ao ma-soeur, ao baba, ao mama wa jamaa, na zaidi wababa na wamama wa njia ya tatu, watapashwa kukataa peupe mafundisho hayo.
   b) Siku moja tu, wataungama peupe vilevile imani ya Eklezya Katolika ya Kristu.
   c) Kukataa udanganyifu na kuungama imani itafanika mbele ya Askofu ao mjumbe wake.
   d) Wajamaa wako wakristu sawa na wakristu wote; wanapashwa kupatana na wakristu wa paroisse yao, na kutumika pamoja nao kwa kujenga, kuendelesha na kukomesha ushirika mzima wa wakristu.
      Maneno hayo, wajamaa -sawa makundi mingine- hawatakusanyika wakati wakristu wa paroisse wanapokusanyika.
   e) Wababa na wamama wa njia ya tatu wanakataswa kuenda kufundisha wajamaa wengine, isiyo katika paroisse, ao mgini, ao diocèse yao, bila ruhusa ya Askofu mwenyewe ao mjumbe wake.

## KUKATAA UDANGANYIFU
(Abjuration)

Wandugu wapenzi, wababa na wamama,

Eklezya Katolika anaarifu peupe ya kama mafundisho na zoezo zenyi kufuatana hapa, hawapatani hata kidogo na imani na tabia yetu ya sisi wakristu:

- Jamaa yeye moja ni Eklezya ya kweli;
- tukilota, ni kila mara Mungu anavetuonyesha mapenzi yake;
- hali ya ndoa ni hali moja tu ya kweli kwa wakristu;
- ushirika na watu ni ya kweli tu wakipatana sawa bibi na bwana.

Maneno hayo,

1. Unakataa kusema na kufundisha ya kama kundi la jamaa ni yeye moja Eklezya ya kweli?

Jibu: Nakataa.

2. Unakataa kusema na kufundisha ya kama tukilota ni kila mara Mungu anayetufumbua mawazo yake?

J/. Nakataa.

3. Unakataa kusema na kufundisha ya kama hali ya ndoa ni yeye moja hali ya kweli kwa wakristu?

J/. Nakataa.

4. Unakataa kusema na kufundisha ya kama ushirika na watu unapashwa kutimilizwa katika hali ya bibi na bwana kwa kuwa wa kweli?

J/. Nakataa.

5. Unakataa kusema na kufundisha ya kama Bikira Maria ndiye mtu wa kwanza Mungu aliyekusudia katika mawazo yake, mbele ya Kristu mtu?

J/. Nakataa.

[illegible]. Unakataa kusema na kufundisha, sawa wababe na [illegible] wengine wanaofundisha, ya kama Bwana Yesu alipatana katika mwili na mama wake Maria; ya kama alipatana vilevile hivi na Maria Madalena na wamama wengine wanaotajwa katika Enjili?

J/. Nakataa.

7. Unakataa mafundisho yote na ufasiri wa uwongo juu ya Bikira Maria aliyeshirika katika mwili na Yoane na Mitume wengine?

J/. Nakataa.

8. Unakataa kusema na kufundisha ya kama ubatizo wa kweli ni mpaka ubatizo na maji yenyi kuchangwa na maji ya uzima?

J/. Nakataa.

9. Unakataa kutaja kazi ya ndoa nyumbani na neno la MISA, KOMUNYO, ao KONSEKRASYO, kwa sababu katika Eklezya, Misa, Komunyo na Konsecrasyo iko na maana yake peke yake?

J/. Nakataa.

10. Unakataa kusema na kufundisha ya kama kutoleana mawazo, hasa makosa, kwa wenzake (baba, mama, bibi ao bwana) ni maungamo ya kweli; na ya kama haina tena lazima na padri kwa kuondolea zambi kwa jina la Mungu na Eklezya?

J/. Nakataa.

11. Unakataa kukufura maji ya baraka, ukichanga na maji ya uzima?

J/. Nakataa.

12. Unakataa kugeuza masala ya Eklezya na kuwaelezea namna isiyokupatana na imani na tabia ya sisi Wakristu?

J/. Nakataa.

## KUUNGAMA IMANI

1. Unasadiki ya kama Kristu ni mtu wa kwanza Mungu amekusudia katika mawazo yake mbele ya Bikira Maria?

J/. Nasadiki.

2. Unasadiki ya kama Roho Mtakatifu mwenye kuunganisha ushirika wa Eklezya anaweka vipaji vyake vyote katika Eklezya chini ya hukumu na uwezo wa Mitume na Waaskofu wanaowapyana?

J/. Nasadiki.

3. Unasadiki ya kama Bikira Maria, Mama wa Kristu, hakumjua mume hata mara moja, ao kuzaa watoto wengine?

J/. Nasadiki.

4. Unasadiki ya kama Kristu aliweka Eklezya nzima chini ya Petro, Mitume na Waaskofu, wapate kuiongoza na kuihukumu na uwezo?

J/. Nasadiki.

5. Unasadiki ya kama katika Eklezya wakubwa wake, wao peke, walipewa kwa Kristu ruhusa na uwezo kwa kueleza na kufasiria maana ya Maandiko Takatifu?

J/. Nasadiki.

6. Unasadiki ya kama, katika Eklezya, ubatizo na maji tu, unazaa watoto wa Mungu?

J/. Nasadiki.

7. Unasadiki ya kama kubatiza mara ya pili, kiisha ubatizo wa Eklezya, ni ukufuru?

J/. Nasadiki.

8. Unasadiki ya kama Padri, wenye kupewa Sakramenta ya Upadirisho na uwezo kwa Askofu wake, anaweza yeye peke tu kuondolea zambi na kupatanisha wakosefu na Mungu na Eklezya?

J/. Nasadiki.

9. Unasadiki mafundisho ya Eklezya yenye kutufundisha ya kama katika ndoa bwana na bibi wanaunganishwa kwa lote, na katika sheria ya Mungu inakataswa bwana akusudie kumtolea bibi kwa bwana mwingine, ao bibi kumtolea bwana kwa bibi mwingine?

J/. Nasadiki.

10. Unasadiki ya kama wazazi wako na [illegible] kubwa sana ya kuwadibisha na kuwafundisha watoto wao wa mwili; basi kuwachilia kwa ajili ya watoto wa roho ni kukosea mapashwa ya ndoa?

J/. Nasadiki.

## SALA YA MWISHO

Mungu Mwenyezi, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu,
umetuzaa kuwa watoto wapya katika Ubatizo,
umetuondolea zambi zote tukitubu;
tunakuomba:
utuchunge ndani ya Bwana wetu Yesu Kristu, kwa uzima wa milele.

J/. Amen.

Ilifanyika pa Lubumbashi, 20-1-1973.

Akina Askofu KABANGA, Askofu mkuu wa Lubumbashi.
Akina Askofu KABANGU, Askofu wa Luebo.
Akina Askofu KABWE , Askofu wa Manono.
Akina Askofu KANYAMA, Askofu wa Kabinda.
Akina Askofu MALUNGA, Askofu wa Kamina.
Akina Askofu LEROY, Askofu wa Kilwa.
Akina Askofu MUKENGE, Askofu wa Luiza.
Akina Askofu MULOLWA, Askofu wa Kalemie-Kirungu.
Akina Askofu NDAY, Askofu wa Kongolo.
Akina Askofu YUNGU, Askofu wa Tshumbe.
Monseigneur NAWEJI, Vicaire Général wa Kolwezi.